# BARAZA LA WAWAKILISHI
# ZANZIBAR

**Simu ya Upepo: Baraza**
**Nambari ya Simu:2230234/5**
**Tele Fax. Nam. (024)2230215**

**SANDUKU LA BARUA 902,**
**ZANZIBAR**

## KAMATI YA KUDUMU YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA

**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2011/2012**

**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambapo katika ripoti hii inajulikana kama "Kamati" ni moja wapo ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi – Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar, 1984 na kuundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 104 (f) ya Kanuni za Baraza la Wawakilkishi - Zanzibar, Toleo la 2011. Kazi na majukumu ya Kamati hii yameainishwa na kufafanuliwa kwenye Kanuni ya 111 ya Kanuni za Baraza.

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inawajibika kufuatilia utekelezaji wa Wizara mbili za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni pamoja na Idara na Vitengo vilivyochini ya Wizara hizo. Wizara zinazosimamiwa na Kamati ni kama zifuatazo:-

i. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

ii. Wizara ya Katiba na Sheria.

**MPANGILIO WA KAZI**

Kiujumla, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita (6) kwa utaratibu ufuatao.

i) Pemba kuanzia tarehe 26/09/2011 hadi 07/10/2011

ii) Unguja kuanzia tarehe 12/12/2011 hadi 23 /12/2011

iii) Pemba na Unguja kuanzia tarehe 20/02/2012 hadi 25/02/2012 kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 28 /02/2012 hadi tarehe 02 /03/2012 kwa upande wa Unguja.

Katika kutekeleza shughuli zake kwa kipindi hiki, pamoja na mambo mengine, Kamati iliweza kufuatilia yafuatayo:-

i) Utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliotolewa kwenye ripoti ya mwaka wa fedha 2010/2011.

ii) Utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara mbili zilizotajwa hapo juu kwa mujibu wa malengo waliyoyawasilisha Barazani kupitia Hotuba za Bajeti za Wizara hizo.

iii) Taarifa ya mapato na matumizi na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliochini ya Wizara zilizochini ya Kamati hii kwa kipindi kilichotajwa hapo juu.

**WAJUMBE WA KAMATI**

Kwa kipindi hicho, Kamati hii iliundwa na Wajumbe saba na Makatibu wawili. Wajumbe wote walishiriki vyema na kikamilifu kwenye shughuli za Kamati mwanzo hadi mwisho. Napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru kwa mashirikiano yao makubwa ambayo yameiwezesha Kamati ya

Katiba, Sheria na Utawala kufanya shughuli zake kwa ufanisi mkubwa. Orodha kamili ya majina ya Wajumbe wa Kamati hii ni kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Abdalla Ali | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Panya Ali Abdallah | - | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Suleiman Hemed Khamis | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Wanu Hafidh Ameir | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mussa Ali Hassan | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Ismail Jussa Ladhu | - | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Nasra Awadh Salmin | - | Katibu |
| 9. | Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi | - | Katibu |

**MUUNDO WA RIPOTI.**

Ripoti hii inatoa kwa muhtasari taarifa za utekelezaji wa Wizara, Vitengo na Idara zilizochini ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kama zilivyoainishwa na Wizara husika kwa Kamati zikionesha utekelezaji halisi (mafanikio) na vikwazo vinavyo zikabili. Aidha, maoni na mapendekezo ya Kamati yametolewa baada ya mjadala na mazingatio ya taarifa hizo kwa lengo la kukuza ufanisi na kuongeza uwajibikaji ndani ya Serikali.

Hivyo, ripoti hii imegawika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza inahusu Utangulizi ambao unajumuisha Utangulizi wenyewe, Mpangilio wa Kazi, Wajumbe wa Kamati pamoja na Muundo wa Ripoti. Sehemu ya pili inagusia zaidi hatua zilizofikiwa katika utekelezaji halisi wa malengo kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sehemu ya tatu inaelezea utekelezaji wa malengo kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Sehemu ya nne ni hitimisho pamoja na maoni ya jumla ya Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## WIZARA YA NCHI, (OR), UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 ilitekeleza mambo yafuatayo:-

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI.**

Kwa kipindi hicho Idara hii imefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo;-

1. Kutayarisha rasimu ya Sera ya Usafiri yenye lengo la kuweka mfumo bora wa usafiri utakaohakikisha kuwepo kwa taratibu na miongozo ya upatikanaji wa huduma za usafiri kwa Watumishi wa Umma. Rasimu hiyo inatarajiwa kupelekwa kwa wadau Unguja na Pemba ili kupata michango yao.

2. Kuwawekea mazingira mazuri Watumishi wa Umma na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla, ambapo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Afya na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na Shirika la Bima zimeendelea na matayarisho ya utafiti ambao utawezesha kuanzishwa kwa mfumo wa Bima ya Afya Zanzibar. Hadidu rejea ya utafiti huo zimekamilika.

3. Kutayarishwa Muongozo na Hadidu rejea za Sera ya mawasiliano ya elektroniki. Kukamilika Sera hii kutaiwezesha Serikali kuingia katika mfumo wa kisasa wa utoaji huduma kwa umma.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Katika mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2011 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 68,603,500/- sawa na asilimia 94 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

**Changamoto**
Katika uratibu na ufuatiliaji wa Programu ya Mageuzi ya utumishi wa umma umeonesha kuchelewa kwa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa katika Programu kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kutokana na kuchelewa kwa uingizwaji wa fedha kutoka Benki ya Dunia.

**Maoni ya Kamati.**
Kamati inashauri kuharakishwa kwa mfumo wa Bima ya Afya kwa kua mfumo huu ndio mkombozi wa upatikanaji wa huduma bora. Hivyo, Wizara hii kwa kushirikiana na Wizaraya ya Afya pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar zichukue hatua za haraka katika kufanikisha suala hilo.

**IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI.**
Kwa kipindi hicho Idara hii ilitekeleza yafuatayo;-

1. Ilichapisha vipeperushi vya Mradi wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma.

2. Ililipia shughuli za uendeshaji wa programu ya mageuzi ya Utumishi wa Umma.

3. Ilihudumia shughuli za kawaida za Wizara zikiwemo ununuzi wa samani, Kompyuta na Fotokopi.

4. Ilitayarisha na kukamilisha Kanuni za Sheria ya Utumishi wa Umma baada ya kupata maoni kutoka kwa wadau mbalimbali. Hatua inayofuata ni kuziwasilisha Kanuni hizo kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu kabla ya kuziwasilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili zianze kutumika rasmi.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**
Katika mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2011 Idara hii iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 246, 325,592/- sawa na asilimia 110 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

**Maoni ya Kamati.**
Kamati inashauri Wizara hii izidishe mawasiliano na Wizara nyengine za SMZ ili kutoa taarifa za mabadiliko na mageuzi ya utumishi Serikalini ili kupunguza migongano na kuweka uwiano katika Utumishi.

**IDARA YA UTAWALA BORA.**
Kwa kipindi hicho, Idara hii imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo;-

1. Ilitayarisha Sera ya Utawala Bora, ambayo ilipelekea kuandaliwa kwa Mswada wa Kuzuia Rushwa, ambao umeshawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi wa Januari, 2012 na Sheria ya Maadili ya Viongozi ambayo ipo katika hatua za mwisho kukamilika.

2. Katika kuwajengea uwezo wananchi juu ya dhana nzima ya uelewa wa Utawala Bora, elimu ya uraia kwa umma kupitia vipindi vya redio, semina na makongamano imetolewa na jumla ya vipindi saba (7) vimerushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar.

3. Katika kutatua kero mbali mbali za wananchi jumla ya malalamiko matatu (3) kutoka kwa wananchi wa kawaida na watumishi yamefanyiwa kazi.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**
Katika mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2011 Idara ya Utawala Bora iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 16,090,346/- sawa na asilimia 50 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

**Maoni ya Kamati.**

1. Idara ya Utawala Bora kutembelea Vyuo vya Mafunzo ili kuona yanayotendeka katika Vyuo hivyo.

2. Kamati inashauri kuongezwa kwa vipindi vya kuwaelimisha Wananchi juu ya Elimu za Uraia na Utawala Bora ili wananchi waweze kujua haki zao.

3. Kuingiza katika mitaala ya skuli somo la Haki za Binaadamu na Utawala Bora.

4. Kuipatia ufumbuzi migogoro ya Ardhi kati ya wananchi na wawekezaji na pia kati ya wananchi na viongozi na watendaji wa Serikali.

5. Malalamiko kuhusu Askari wa Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi kuingilia kazi za Polisi na kuwanyanyasa raia.

6. Rushwa katika mahakama hasa kwa baadhi ya Mahakimu ambapo kunaathiri utoaji wa haki na kukosekana uadilifu katika kushughulikia kesi.

7. Haja ya sifa zinazotumika katika uteuzi wa Masheha kuwekwa wazi.

**IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA**

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 Idara hii imeweza kutekeleza malengo yafuatayo;-

1. Katika kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi, Idara ya Nyaraka imenunua vifaa mbali mbali vya Ofisi ikiwemo; Kompyuta na samani.

2. Katika kuwahudumia Watafiti mbalimbali wanaofika Idarani hapo, Idara imehudumia jumla ya Watafiti 133, ambapo kati ya hao 109 ni Watanzania, na 24 ni Wageni kutoka nchi mbalimbali za nje.

3. Imekusanya kumbukumbu tuli, imetoa ushauri na maelekezo muhimu kuhusiana na mfumo bora wa Utunzaji na Uhifadhi kumbukumbu katika Wizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali kumi na nane (18) Unguja na Pemba.

4. Katika kuimarisha usalama wa Jengo la Nyaraka, Maofisa wawili wamefanya ziara ya kikazi huko Dar es salaam kwa lengo la kukagua mitambo ya CCTV inayotarajiwa kufungwa katika Ofisi ya Nyaraka - Unguja.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Katika mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2011 Idara hii iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 17,761,045/- sawa na asilimia 58 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

Kwa upande wa Pemba **Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa** iliweza kutekeleza majukumu yafuatayo;-

1. Imekusanya kumbukumbu zote ambazo zimefikia umri na kuhamishiwa jengo la Nyaraka za Taifa (Archives) kwa ajili ya kupatiwa hifadhi ya kudumu na kuzifanyia tathmini na kuziingiza katika mwongozo (Archive guide) tayari kwa kutoa huduma kwa jamii kwa kiwango kinachotakiwa. Ofisi ambazo zimekusanywa kumbukumbu hizo ni Wizara ya Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini - Pemba na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Chake chake.

2. Katika kuimarisha uhifadhi wa kisasa na wakitaalamu wa kumbukumbu, njia mbadala (Backup Storage) imeanzishwa kwa kuziingiza kumbukumbu kwenye mfumo wa *Digital*. Jumla ya majalada 8,677 yameingizwa katika mfumo wa huo.

3. Iliendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa Uhifadhi wa Kumbukumbu kwa Watumiaji/Watoa maamuzi (decission maker) na Wahifadhi kumbukumbu (Records Staff) kwa masjala za Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini - Pemba, Ofisi ya Mrajisi wa Serikali, Wizara ya Afya, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkoani, Baraza la Mji Mkoani, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake chake.

4. Iliweza kutoa huduma kwa watumiaji wa kumbukumbu wa ndani na nje ya Nchi. Jumla ya watumiaji 36 wa ndani, na sita (6) kutoka Nchi za nje waliweza kuhudumiwa.

**Maoni ya Kamati.**
Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inashauri yafuatayo;-

1. Serikali kwa kupitia Wizara husika itafute eneo kwa lengo la kujenga Ofisi mpya hasa ukizingatia kwamba eneo iliopo sasa ni dogo na pia limezungukwa na majengo ya wananchi.

2. Malipo yote ya Tafiti zinazofanywa katika Idara ya Nyaraka zilipwe moja kwa moja Idarani hapo hasa ukizingatia kuwa wao ndio wasimamizi wakuu wa zile huduma zinazotolewa pale.

3. Jengo la Nyaraka Pemba lipo katika hali mbaya sana kwa hiyo tunaiomba Serikali iwapatie Idara hii jengo la zamani la Mkuu wa Mkoa ili shughuli za Ofisi ziendelee kwa ufanisi zaidi.

4. Kuharakishwa kwa zoezi la kuzihamisha nyaraka kutoka katika mfumo wa *analogy* na kwenda katika mfumo wa digital ili ziweze kudumu kwa muda mrefu zaidi.

5. Kununuliwa kwa kifaa maalumu cha udhibiti wa hali ya hewa ili kiweze kuzuia unyevu wakati kinapowashwa kipoza hewa katika sehemu ya kutunzia nyaraka.

6. Kupatiwa usafiri ili kuweza kupunguza uzito wa kazi za kutembelea Wizara zote za Serikali Zanzibar kwa lengo la kukusanya kumbukumbu na kuzipeleka katika Idara ya Nyaraka kwa kuhifadhiwa kitaalamu zaidi.

**CHUO CHA UTAWALA WA UMMA.**
Katika kipindi hicho Chuo cha Utawala wa Umma kimetekeleza majukumu yafuatayo;-

1. Kimeaandaa muundo wa utumishi wa Chuo pamoja na bajeti ya Chuo inayojumuisha viwango vipya vya mishahara na kuviwasilisha Wizarani baada ya kupitishwa na Baraza la Chuo.

2. Kimepitia na kufanya marekebisho Mitaala ya masomo ya Diploma ya Rasilimali Watu, Utawala wa Umma na Mtaala wa mafunzo ya Cheti cha Sheria.

3. Kimefanya vikao vya Baraza la Chuo ambalo lilijadili na kupitisha matokeo ya Wanafunzi pamoja na kupitia miundo ya Utumishi ya Chuo.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**
Katika mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2011 Chuo cha Utumishi wa Umma kiliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 142,243,589/- sawa na asilimia 61 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI**
Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 Tume ilitekeleza majukumu yafuatayo;-

1. Imefanya kikao cha uzinduzi wa Bodi ya Tume ya Utumishi Serikalini.

2. Imenunua vifaa mbalimbali vya ofisi.

3. Imefanya Mikutano mbalimbali ya kuelimisha Watumishi wa Serikali juu ya Sheria mpya ya Utumishi wa Umma.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**
Katika mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2011 Tume ya Utumishi Serikalini iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 23,000,000/- sawa na asilimia 72 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

**KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA**
Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilipokutana na Makamishna wa Kamisheni hii ilielezwa kuwa; Kamisheni ya Utumishi wa Umma imeandaa Mpango Mkakati '*Strategic Plan'* wa miaka mitano (2011 – 2016) ili Kamisheni iweze kutekeleza vyema majukumu.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Kamisheni ya Utumishi wa Umma hadi Disemba, 2011 iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 46,000,000/- sawa na asilimia 350.

**CHANGAMOTO NA MAONI YA KAMATI**

Kutokana na kutokuwepo kwa maandalizi ya kutosha wakati wa kuanzishwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma zifuatazo ni changamoto za Kamisheni hii;-

1. Uhaba wa Watendaji; katika kutatua hili Kamati inashauri kuajiriwa Watendaji wenye sifa ili Kamisheni iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.
2. Uelewa mdogo wa Sheria ya Utumishi wa Umma kwa Makamishna; katika kufanikisha hili Kamati inashauri kupatiwa taaluma ya Sheria hii Makamishna kwa kuwa ndio kitendea kazi kikuu cha Kamisheni.
3. Ukosefu wa jengo la kudumu la ofisi; tunashauri Kamisheni kupatiwa jengo lao la kudumu hasa tukizingatia kuwa ofisi wanayofanyia shughuli zao hivi sasa ni finyu.
4. Maslahi madogo kwa Makamishna; Kamati inashauri kupatiwa maslahi wanayostahiki Makamishna ili kulinda hadhi yao.

Hivyo, tunaishauri Serikali kufanya maandalizi ya kutosha endepo itaanzisha jambo ili kuepusha usumbufu kwa watendaji wake.

**IDARA YA MAFUNZO NA MAENDELEO YA WATUMISHI.**

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 Idara hii imemudu kutekeleza mambo yafuatayo;-

1. Imeanzisha vitengo vya mafunzo katika kila Wizara Unguja na Pemba, ambavyo vitawezesha kuwa na uratibu mzuri wa mafunzo kwa watumishi wa umma.
2. Imeendelea kuratibu mafunzo ya muda mfupi na ya muda mrefu kwa Watumishi wa Serikali. Jumla ya watumishi (95) wamehudhuria mafunzo mafupi, ambapo nchini India walihudhuria Watumishi (33), Korea (18), Singapore (4), China (9), Japan (2) na Tanzania Bara - ESAMI (24). Kwa upande wa mafunzo ya muda mrefu jumla ya watumishi (5) wamehudhuria mafunzo ya shahada ya pili, ambapo nchini China walihudhuria Watumishi (2), Japan (1) na India (2).

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Katika mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2011 Idara hii iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 9,832,500/- sawa na asilimia 97 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

**IDARA YA MIUNDO YA TAASISI, UTUMISHI NA MASLAHI YA WAFANYAKAZI.**

Katika kipindi hicho Idara hii imefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo;-

1. Imeipitia Miundo ya Utumishi na kuifanyia marekebisho ili kuwawezesha watumishi kuzitambua daraja zao, mishahara wanayostahiki kupata pamoja na utaratibu wa upandishwaji wa vyeo.
2. Imetayarisha Muongozo wa Uhakiki wa wafanyakazi na mishahara, ambao utasaidia kuwatambua wafanyakazi halali wa Serikali na kupelekea kudhibiti upotevu wa fedha kwa malipo ya mishahara.
3. Imetayarisha Fomu ya Upimaji Utendaji kazi na Muongozo wa Mkataba wa Utoaji wa Huduma kwa mteja utakaosaidia kutambulisha huduma zinazotolewa na taasisi za Serikali na ubora wa huduma inayotolewa.

**Maoni ya Kamati.**

1. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwaongezea maslahi watumishi wa Umma na kuwafanya na wao wajisikie ni moja kati ya wanaonufaika na kodi za Serikali pamoja na nguvu zao wanazozitoa kwa kujenga nchi. Hata hivyo, inashauri kuzidi kufanyiwa kazi zoezi hili ili kuepusha malalamiko yasiyo ya msingi.

2. Kamati inasisitiza kuwepo kwa mawasiliano (network) ndani na nje ya Wizara ili wananchi wapate kuelewa mabadiliko na mwenendo mzima wa Serikali.

3. Kamati inasisitiza kuwepo kwa usawa wa kimaslahi kati ya watendaji wa Serikali wanaotumikia Unguja na wale wanaotumikia Pemba, kwani kumebainika kuwa kuna tofauti kubwa ya mishahara baina ya Watendaji hao. Kwa mfano; mfanyakazi anayefanya kazi ya Uhasibu - Unguja analipwa kulingana na elimu yake na muda wa kazi aliotumikia ila kwa upande wa Pemba hulipwa kwa mujibu wa elimu yake pekee. Jambo hili linaleta migongano baina ya wafanyakazi wa Unguja na wale wa Pemba.

4. Kamati inashauri Idara hii kuvitumia vyombo vya habari kama TV na Redio ili watumishi wazijue huduma zinazotolewa na Idara husika.

**IDARA YA MIPANGO YA RASILIMALI WATU.**
Katika kipindi hicho, Idara hii imejitihidi kutekeleza majukumu yafuatayo;-

1. Kuimarisha kumbukumbu za Watumishi wa Umma, ambapo Idara imeanzisha Mfumo wa uwekaji wa taarifa za Rasilimali Watu ambao utasaidia kuweka na kuzitumia taarifa hizo katika masuala ya kiutumishi zikiwemo mahitaji ya watumishi, taaluma zao na kuweka makisio ya wastaafu pamoja na muelekeo wa mafao yao.

2. Imekamilisha zoezi la kuorodhesha vijana walioomba kazi kwa kuainisha viwango vyao vya elimu na fani walizosomea kwa lengo la kufanya mazingatio ya mipango ya baadae.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**
Katika mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2011 Idara hii iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 11,000,000/- sawa na asilimia 44 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

**OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI.**
Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 Ofisi hii imefanikiwa kutekeleza majukumu yafuatayo;-

1. Imeendelea kuwawekea mazingira mazuri Watumishi wake ambapo, Ada ya masomo pamoja na gharama nyengine zimelipwa kwa wafanyakazi 21 waliojiunga na Chuo kwa mwaka wa masomo 2011/2012 na wafanyakazi 17 wanaoendelea na masomo yao katika vyuo mbalimbali.

2. Jengo jipya lililonunuliwa limefanyiwa matengenezo na kuweka laini za umeme, kupiga plasta pamoja na kuweka milango na madirisha.

3. Kazi za ukaguzi za mwaka 2009/2010 zinaendelea katika Taasisi mbali mbali za Serikali kwa kufuata muongozo wa ukaguzi. Aidha, Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka 2008/2009 imekamilika na tayari imeshawasilishwa Serikalini.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**
Katika mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2011 Ofisi ya Mdhibiti iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 404,939,666/- sawa na asilimia 123 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

Kwa upande wa Pemba **Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar** kwa kipindi hicho kilitekeleza malengo yafuatayo;-

1. Kufanya mapitio Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa Ofisi wa mwaka 2011 – 2014.

2. Kufanya mapitio ya muongozo wa ukaguzi (Audit Manual) ili kujenga uwezo wa wafanyakazi katika kufanya ukaguzi wa kisasa.

3. Kufanya Mkutano Mkuu wa mwaka ambao lengo lake ni kufanya tathmini ya utendaji kazi za mwaka uliopita na kuweka maazimio ya mpango kazi kwa kazi za mwaka unaofuata.

4. Kufanya kazi za ukaguzi wa hesabu za mwaka 2010/2011.

5. Kuendelea kuwalipia gharama za masomo wafanyakazi wake kumi na nne waliopo masomoni.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2012 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu - Pemba iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 258,454,000/- kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo. Fedha za mishahara ni shilingi 147,884,000/- na matumizi mengineyo ni shilingi 110,570,000/-.

Hata hivyo, kwa kipindi hicho Ofisi hii iliingiziwa jumla ya shilingi 129,494,119/- sawa na asilimia 26.11, kati ya fedha hizo shilingi 67,494,119/- sawa na asilimia 26.11 ni kwa mishahara na shilingi 62,000,000/- sawa na asilimia 23.99 ni kwa ajili ya matumizi mengineo.

**Maoni ya Kamati.**

Kamati inashauri ripoti zote za Mawizara ziwe zinajadiliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali akishirikiana na Waziri wa Wizara husika pamoja na Rais kwa msaada wa Waziri wa Utumishi na Utawala Bora ili kuongeza umakini katika matumizi na mapato ya Serikali.

**UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA - PEMBA**

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2012 Wizara hii kwa upande wa Pemba kupitia Taasisi zake mbali mbali ilitekeleza mambo yafuatayo;-

1. Imeendelea na utoaji huduma za kiutawala kwa Rasilimali Watu (Administrative Service to the Staff), ambapo huduma mbali mbali za kuendeshea kazi zimefanywa kwa lengo la kuimarisha ubora wa nguvu kazi na kuweka mazingira mazuri ya kazi.

2. Iliendelea kuwajengea uwezo na kuwaendeleza wafanyakazi wake, ambapo jumla ya Wafanyakazi watano **(**5**)** wamepatiwa nafasi za masomo kwa fani tofauti. Jadweli lifuatalo linaonesha mchanganuo huo.

| IDADI YA WAFANYAKAZI | KIWANGO/ FANI | CHUO WANACHOSOMA |
|---|---|---|
| 1 | Digrii ya pili ya Uhasibu | IAA |
| 2 | Diploma ya U/Kumbukumbu | Chuo cha Utawala wa Umma |
| 1 | Diploma ya Rasilimali Watu | Chuo cha Utawala wa Umma |
| 1 | Cheti – Umeme | Chuo Amali - Vitongoji |

3. Katika kuweka mazingira bora ya kazi, Ofisi imefanya ununuzi wa mashine, samani na vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.

4. Kwa kushirikiana na Ofisi kuu Unguja, Ofisi hii imeweza kuandaa semina ya sera ya mawasiliano ya Serikali kwa njia ya elektroniki (e - Government). Sera hii itakapokamililika itawasaidia wananchi kupata huduma ya mawasiliano kwa urahisi.

5. Imetayarisha mpango wa matumizi ya muda wa kati - MTEF wa Ofisi.

6. Kwa kushirikiana na Ofisi kuu Unguja, Ofisi hii imetayarisha rasimu ya awali ya Sera ya Usafiri kwa Viongozi, Watendaji Wakuu na Watumishi wengine wa Umma. Sera hii ina dhamira ya kuweka miongozo, utaratibu na mipango maalum itakayohakikisha upatikanaji, ugawaji, usimamizi, uhifadhi, utumiaji mzuri wa vyombo vya usafiri, safari za Watumishi wa Umma na upatikanaji wa mikopo itakayowawezesha Watumishi wa Umma kwa mujibu wa dhamana zao.

7. Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi kuu Unguja imefanya uhakiki pamoja na ukaguzi wa malipo ya mishahara (Pay - Roll) ya wafanyakazi kwa Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

8. Katika kutoa miongozo juu ya usimamizi na utekelezaji wa sheria mbali mbali za uendeshaji wa utumishi wa umma, Ofisi imefanya ziara kwa Wizara 16 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kutoa muongozo juu ya usimamizi na utekelezaji wa sheria mbali mbali za uendeshaji wa utumishi wa umma.

9. Iliweza kutoa uhamisho wa kiwizara, kubadilisha kada, kuwapokea na kuwapangia kazi wafanyakazi wanaorudi masomoni. Aidha, ilifanya marekebisho ya mishahara kwa wafanyakazi wanaorudi masomoni.

10. Kwa kushirikiana na Ofisi kuu Unguja, Ofisi hii imefanikiwa kutoa mafunzo kwa maafisa utumishi wa Wizara na taasisi za umma juu ya namna bora ya matayarisho ya makisio ya mishahara (Nominal Roll).

11. Imeweza kukusanya maoni (data input) juu ya uanzishwaji wa mfumo wa uwekaji wa taarifa za watumishi wa Umma (Central Human Resource Data Base) katika Wizara na Taasisi za Serikali kwa lengo la kuutambulisha na kuuboresha zaidi uanzishwaji wa mfumo huo. Jumla ya Taasisi 6 za Serikali zilipitiwa katika zoezi hilo. Taasisi zenyewe ni:- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Wizara ya Afya, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka ya Maji na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

12. Imeratibu na kutoa nafasi za mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi, ambapo jumla ya wafanyakazi watatu wameweza kupatiwa mafunzo hayo nchini china.

13. Imekusanya maoni kwa njia ya madodoso kwa watendaji na viongozi wa taasisi za Serikali kwa ajili ya utayarishaji wa sera ya mafunzo.

14. Katika kuimarisha utawala bora katika Wizara hii, Ofisi hii iliweza kutoa mafunzo ya ndani (In House Training) kwa wafanyakazi wake juu ya ufahamu wa dhana nzima ya Utawala Bora na misingi yake ili wafanyakazi hao waweze kuwa na uelewa wa kutosha juu ya dhana nzima ya Utawala bora.

15. Kwa kushirikiana na Ofisi kuu Unguja, Ofisi hii iliendesha warsha juu ya Rasimu ya Sheria ya Kupambana na Rushwa – Zanzibar, ambayo ililenga kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbali mbali walioko Pemba.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora -Pemba kwa mwaka wa fedha 2011/2012 imeidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 182,770,000/-, kati ya hizo jumla ya shilingi 79,210,000/- ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 103,560,000/- zimetengwa kwa ajili ya matumizi mengineo. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2011, jumla ya shilingi 44,268,000/- ziliingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi mengineo, sawa na asilimia 42.74%

**Changamoto**

Pamoja na ufanisi mkubwa unaopatikana Wizara hii kwa upande wa Pemba inakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

1. Ufinyu wa bajeti.
2. Ukosefu wa vyombo vya Usafiri

## SEHEMU YA TATU

# WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Wizara ya Katiba na Sheria katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 kupitia Taasisi zake mbali mbali ilifanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo;-

## IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 Idara hii imemudu kutekeleza malengo yafuatayo;-

a) Iliandaa Semina elekezi kwa Maafisa Mipango Unguja na Pemba kuhusu MTEF, "Strategic Planning", "Project Proposal" na "Resource mobilization".

b) Imeanza maandalizi ya kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya NGO's kwa kutangaza tenda kwa ajili ya kutafuta Mshauri Elekezi.

c) Katika kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na Tathmini na Utoaji wa taarifa katika Sekta ya Sheria, orodha ya awali ya viashiria imetayarishwa.

d) Katika kuimarisha ubadilishanaji wa taarifa na kutoa elimu kwa umma juu ya sekta ya sheria, vimeandaliwa vipindi ambavyo vitarushwa hewani karibuni.

### Hali ya Upatikanaji wa Fedha

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 74,554,000/- kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Disemba, 2011 jumla ya shilingi 31,076,600/- sawa na asilimia 42 ziliingizwa na kutumiwa.

## IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2012 Idara hii imeweza kutekeleza malengo yafuatayo;-

1. Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma kwa upande wa Wizara kwa;-

    i) Kuanza kutayarisha Mpango wa Rasilimali Watu wa Wizara. Katika kutekeleza hili hatua za msingi zimeanza kuchukuliwa ikiwemo kuwapanga upya wafanyakazi katika taasisi za Wizara.

    ii) Kulipa gharama za mafunzo kwa wafanyakazi wanaoendelea na masomo.

2. Kuratibu kazi za uendeshaji wa Wizara kwa;-

    i) Kulipa gharama za huduma za awali za kuhuisha tovuti na mtandao.

    ii) Kuandaa Mikutano ya Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji na Mikutano mingineyo.

    iii) Kulipa gharama za mafuta ya gari na ‘generator’ pamoja na matengenezo ya gari.

    iv) Kuandaa safari mbalimbali za kikazi kwa Viongozi na Watendaji za ndani na nje ya Zanzibar.

    v) Kununua vifaa vya kutendea kazi, samani na vifaa vya kuandikia.

    vi) Kulipia gharama za mawasiliano na huduma mbalimbali za uendeshaji kama vile ulipaji wa Bili za simu, maji, umeme na huduma mbalimbali za ofisi, ununuzi wa spare nakadhalika.

### Hali ya Upatikanaji wa Fedha

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 438,552,000/- kati ya fedha hizo shilingi 220,442,000/- kwa ajili ya mishahara na maposho na shilingi 218,110,000/- kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Disemba, 2011 jumla ya shilingi 251,140,329/- sawa na asilimia 57 ziliingizwa na kutumiwa. Kati ya hizo shilingi 140,727,732/- kwa ajili ya mishahara na maposho na shilingi 110,412,597/- kwa matumizi mengineyo.

**Changamoto**
Idara hii inakabiliwa na changamoto ya kutoingiziwa fedha za ujenzi wa jengo la Wizara kwa wakati. Kutokana na hili Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaiomba Serikali kuingizia Idara hii fedha za ujenzi huo kwa wakati kwa kuwa fedha za Idara hii tayari zipo.

**MAHKAMA**
Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 Mahakama imeweza kutekeleza malengo yafuatayo;-

1. **Kuimarisha majengo ya Mahkama,** katika kutekeleza hili Mahkama iliendelea kufanya matengenezo katika sehemu ya chini ya jengo lake la Vuga na sehemu ya nje ya jengo la Mahakama Chwaka. Aidha, inaendelea na hatua za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Kadhi huko Mwanakwerekwe.
2. **Kuendelea na hatua za kuanzisha Mahakama ya Biashara**, katika kufanikisha hili Mahakama ilishawasilisha mbele ya Kamati ya Uongozi Sheria na Kanuni za Mahakama ya Biashara, michoro ya ukarabati wa Jengo hilo tayari imewasilishwa na Mkandarasi ameshachaguliwa. Aidha, hatua za kuitisha tenda ya ununuzi wa vifaa vya Ofisi zinaendelea.
3. **Kujenga mazingira bora ya utendaji kazi,** Mahakama katika kuimarisha uwezo wa Watendaji imeendelea kuwalipia masomo wafanyakazi wake watano. Aidha, iliandaa semina elekezi kwa Watendaji wake. Pia, iliendelea kuwapa motisha Wafanyakazi mbalimbali kwa kuwalipa posho la likizo, malipo baada ya saa za kazi, mazishi n.k. Halkadhalika, ilinunua vitendea kazi na kugharamia gharama za kuendeshea ofisi. Vile vile, viongozi mbalimbali wa Mahakama Unguja walifanya ziara za kikazi Unguja na Pemba pamoja na nje ya Nchi.
4. **Kuharakisha mwenendo wa Kesi**, katika kutekeleza hili iliwalipa posho Washauri na Mashahidi pamoja na kuandaa kikao cha Kamati ya Kusukuma Kesi huko Pemba.
5. **Kuimarisha Mahakama ya Kadhi**, katika kufanikisha hili Mahakama imefanikiwa kumpata Mtaalamu wa kuifanyia mapitio Sheria ya Mahakama ya Kadhi na tayari ameanza kukusanya maoni kwa Wadau Unguja na Pemba. Aidha, iliwafanyia semina mbalimbali Makadhi kwa kuwajengea uwezo wa kiutendaji. Pia, iliendelea kuwapa motisha Wafanyakazi mbalimbali kwa kuwalipa posho la likizo, nguo za heshima kwa Makadhi, malipo baada ya saa za kazi, mazishi n.k. Halkadhalika, ilinunua vitendea kazi na kugharamia gharama za kuendeshea ofisi.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**
Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Mahakama hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,324,000,000/- kati ya fedha hizo shilingi 724,000,000/- kwa ajili ya mishahara na maposho na shilingi 600,000,000/- kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Disemba, 2011 jumla ya shilingi 1,086,235,545/- sawa na asilimia 82 ziliingizwa na kutumiwa. Kati ya hizo shilingi 765,435,545/- kwa ajili ya mishahara na maposho na shilingi 320,800,000/- kwa matumizi mengineyo.

Kwa upande wa Pemba **Mahakama** katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2011, ilitekeleza mambo yafuatayo;-

a) Ilipokea mashauri ya jinai 577, ambapo mashauri 208 yalisikilizwa na kutolewa uamuzi. Aidha, mashauri 172 ya madai yalipokelewa ambapo mashauri 35 yalisikilizwa na kutolewa uamuzi.

b) Iliapisha Makadhi wapya wanne kwa lengo la kuimarisha utendaji pamoja na kuwaondoshea wananchi usumbufu.

c) Jumla ya Majaji watatu kutoka Unguja walifika Pemba katika vipindi sita tofauti na kuendelea kusikiliza mashauri yaliyofunguliwa Mahakama Kuu kanda ya Pemba.

d) Iliweza kununua vespa moja kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika majukumu yake ya kazi. Pia imeweza kununua viti kumi na nane (18) vya kisasa. Aidha, iliendelea na utaratibu wa

kukata "partitions" ya vyumba viwili katika Mahakama ya Chake Chake na kutia mpira katika sehemu ya paa yenye zege ambayo inavujisha. Vile vile imeweza kuunga internet kupitia mtandao wa Zanlink katika Mahakama ya Chake Chake. Halkadhalika, ilinunua komputa mbili kwa matumizi ya kazi za kawaida.

e) Iliandaa semina za UKIMWI kwa Makadhi pamoja na kufanya mkutano wa wafanyakazi wote wasiokuwa Mahakimu na Makadhi.

**Mapato na Matumizi**
Katika kipindi kilichotajwa Mahkama – Pemba iliweza kukusanya jumla ya shilingi 4,428,235/-, kati ya hizo shilingi 2,389,925/- ni "court fine" na shilingi 2,038,310/- ni "court fee".

Pia, katika kipindi hicho Mahkama - Pemba ilingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 274,386,106/-, kati ya hizo Tsh. 224,669,131/- ni mishahara na maposho na Tsh. 49,716,975/- ni matumizi mengineyo.

**Changamoto**
Pamoja na mafanikio makubwa yanayopatikana Mahkama inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Miongoni mwao ni:-

- Majengo ya Mahkama bado ni chakavu yanahitaji matengenezo makubwa.

- Ufinyu wa bajeti ya masomo hasa ikizingatiwa kuwa hivi sasa Wafanyakazi wengi wanahamu ya kusoma. Maombi ni mengi lakini uwezo wa kuwasomesha ni mdogo hususan kwa upande wa Pemba.

- Uhaba wa Wafanyakazi wenye taaluma kwa viwango tofauti. Aidha, kwa upande wa Pemba – Mahkama ina upungufu wa wafanyakazi katika sehemu ya uchapaji na Mahakimu.

- Ufinyu wa Bajeti unaopelekea Mahkama kutofikia malengo yake iliyojipangia.

- Mahkama kutokuwa na nyumba za kuishi Majaji, Mahakimu na Makadhi ikizingatiwa na unyeti wa kazi zao wanazozifanya za kila siku.

- Ukosefu wa gari ya majaji wa Mahkama Kuu Pemba

- Ukosefu wa fedha za ukarabati wa Jengo la Mahkama ya Biashara kutoka kwa Mfadhili.

**Maoni ya Kamati**
Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inashauri mambo yafuatayo;-

1. Kuongezwa kwa idadi ya Mahakimu kwani imebaini kuwa baadhi ya Mahakimu wanatoa huduma zaidi ya Mahkama moja. Kwa mfano; Hakimu wa Mkoa wa Mahkama ya Wete inasikiliza kesi za kawaida za Mkoa mzima wa Kaskazini Pemba pamoja na kesi za ardhi za Mkoa huo. Hali hii husababisha mlundikano wa majalada pamoja na kumfanya Hakimu huyo kutekeleza majukumu yake bila ya ufanisi kutokana na mzigo mzito aliokuwa nao.

2. Kwa kuwa baadhi ya Mahakimu hukaa sana kwenye Kituo kimoja cha kazi, Kamati inaishauri Mahkama kuwaondoa kwenye Vituo wale Mahakimu waliotumikia kwa muda mrefu kwenye Kituo kimoja ili kuleta ufanisi bora wa kazi.

3. Makarani wanaowasaidia Mahakimu 'Court Clerk' wapatiwe sare 'uniform' ili na wao waonekane 'smart'. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya Makarani huvaa mavazi yasiyoendana na hadhi yao.

4. Kwa kuwa Mahakimu na Wafanyakazi wa kawaida wa Mahkama wanautumikia mhimili mmoja yaani Mahkama, Kamati inashauri ni vyema watendaji wote hawa wakawa chini ya Tume ya Utumishi ya Mahkama.

5. Kwa kuwa katika Mahkama ya Wilaya ya Mkoani baadhi ya siku Watuhumiwa huwa hawafikishwi Mahkamani hapo na baadhi ya siku hufikishwa mchana. Hali hii hupelekea kuwakosesha Watuhumiwa haki yao ya dhamana. Hivyo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inalishauri Jeshi la Polisi kuandaa mpango madhubuti ili kuondosha tatizo hilo.

6. Kwa kuwa jengo la Mahkama ya Wilaya ya Mkoani nafasi yake ni finyu na jambo hili hupelekea Wafanyakazi wa Mahkama hii kuchanganyika na Watuhumiwa na kwa kuwa Mahkama hii ina eneo (kiwanja) la kujenga ni vyema Serikali ikaingiza fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahkama hii ili kuondosha tatizo hilo.

**AFISI YA MWANASHERIA MKUU**

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 Afisi ya Mwanasheria Mkuu imemudu kutekeleza majukumu yafuatayo;-

1. Ilifanya marekebisho ya muundo na mfumo wa Utendaji wa Afisi, katika kutekeleza hili Afisi hii iliandaa mikutano ya ndani kwa ajili ya kubainisha “Core and Non Core functions” za Utendaji, vitengo muhimu vya Ofisi na kutambua idadi ya ongezeko la Watendaji wanaohitajika kwa mujibu wa Vitengo husika.
2. Ilinunua vitendea kazi kwa mujibu taratibu za manunuzi.
3. Iliandaa nyaraka mbali mbali ambazo zinatumika katika kuendesha kazi za kila siku za kila Kitengo.
4. Iliandaa vikao vya Bodi ya Zabuni ya ununuzi wa gari pamoja na vikao vya Kamati ya Msamaha wa Rais.
5. Iliweka Mfumo wa Mawasiliano wa Mtandao (Installation of Dedicated Bandwith and Wireless Internet Services). Kazi hii imerahisisha mawasiliano kati ya watendaji wa Taasisi hii na Taasisi nyengine za Serikali.
6. Imekamilisha taratibu za kumpata Mzabuni wa Ununuzi wa Gari ya Afisi.
7. Imeandaa mapendekezo ya kusomwa kwa Miswaada mara tatu kabla ya kupitishwa na Baraza la Wawakilishi na kuwa sheria.
8. Kazi ya Ujenzi wa Makao Makuu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika hatua ya pili imeanza kwa kunyanyua kuta ya ghorofa ya kwanza.
9. Imetayarisha waraka wa mapendekezo ya Muundo wa Kitengo cha Mikataba na kuwasilisha waraka Wizarani, Kamati ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mapinduzi kwa kujadiliwa.
10. Ilichapisha Sheria za Zanzibar kuanzia mwaka 1980 hadi 2010.
11. Ilimpata Mshauri Mwelekezi wa kuzipitia Sheria za Zanzibar na kuziweka pamoja (Consolidation) ambapo ameshawasilisha taarifa ya awali ya kazi hiyo.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Afisi hii iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 612,077,000/- kati ya fedha hizo Tsh. 137,216,000/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 474,861,000/- kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Disemba, 2011 jumla ya Tsh. 346,276,973/- sawa na asilimia 57 ziliingizwa na kutumiwa. Kati ya hizo Tsh. 84,476,973/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 261,800,000/- kwa matumizi mengineyo.

**Changamoto**

Pamoja na mafanikio mbali mbali yanayopatikana Afisi hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

a) Ufinju wa nafasi katika jengo lake.

b) Uhaba wa Watendaji.

**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA**

Kwa kipindi cha Julai, 2011 hadi Disemba, 2012 Tume ya Kurekebisha Sheria imeweza kutekeleza mambo yafuatayo;-

1. Kuimarisha Afisi yake na kuifanya iwe na hadhi kwa mujibu wa kazi zake kwa;-
   i. Kununua vespa, kiyoyozi 'Air Condition', mashine ya kusafishia 'hover', kabati, printer, laptop, Kompyuta, stand banner, vitabu na vifaa vyengine.
   ii. Kuweka mtandao na kuimarisha mfumo wa mawasiliano.
   iii. Kuanza kuratibu hatua ya kupita katika Mawizara na kujuwa sheria zisizotumika, ili kuweza kuweka takwimu halisi.
   iv. Kufanya matengenezo na huduma nyenginezo.
2. Kuongeza idadi ya Wanasheria na watendaji wengine wa Afisi na kuendelea kuimarisha uwezo na taaluma zao.
3. Kuzipitia Sheria na kupendekeza marekebisho yanayohitaji kufanywa ambapo Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Nam.9/2006 na Sheria ya Ushahidi Sura 5 ya 1917 marekebisho yao yanaendelea na tayari "issuepaper" zimeshasambazwa kwa Wadau.
4. Imeanzisha na kuimarisha mashirikiano na jumuiya mbalimbali zenye majukumu sawa na ya Tume. Kwa kuanzia Watendaji wa Tume wamepata mafunzo kutoka Tume ya Kurekebisha Sheria ya Tanzania Bara.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Tume hii iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 174,914,000/- kati ya fedha hizo Tsh. 38,547,000/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 136,367,000/- kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Disemba, 2011 jumla ya Tsh. 72,338,142/- sawa na asilimia 41 ziliingizwa na kutumiwa. Kati ya hizo Tsh. 22,578,142/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 49,760,000/- kwa matumizi mengineyo.

**Changamoto na Maoni ya Kamati**

Tume ya Kurekebisha Sheria inakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

a) Ukosefu wa jengo la kudumu, kwa hivi sasa Tume imeanzimwa jengo hapo Eacrotanal - Maisara. Hata hivyo, Tume hii inakabiliwa na ufinyu wa nafasi. Ingawa Tume ya Kurekebisha Sheria haikupewa muda maalum wa kulitumia jengo hilo, Kamati inaishauri Serikali kuijengea Tume jengo lake katika eneo walilopewa ili kuepusha usumbufu hapo baadae.

b) Watafiti wa Tume hawana taaluma ya utafiti. Kutokana na hili Kamati inaishauri Tume kuwapatia elimu ya utafiti watendaji hawa ili waendane na wakati sambamba na kufanya shughuli zao kwa taaluma zaidi. Aidha, inawashauri watafiti hawa kuwa 'active' jambo hili litapelekea kutokurekebisha Sheria zetu mara kwa mara.

c) Ukosefu wa Wataalamu wa Uandishi wa Sheria (Draftman).

d) Baadhi ya Mawizara kutoishirikisha Tume wakati wa kufanya mapitio ya Sheria.

**AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2012 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imemudu kutekeleza majukumu yafuatayo;-

1. Kuimarisha na kuendeleza uwezo wa Afisi kiutendaji, Uendeshaji kazi na Rasilimali Watu kwa;-
   i) Kununua vifaa mbalimbali vipya na kufanya matengenezo kwa vifaa vilivyopo.
   ii) Kufanya mafunzo madogo ili kuimarisha mfumo wa data base.

iii) Kuchapisha na kusambaza ripoti ya mwaka juu ya Uendeshaji Mashtaka ambapo hatua za awali zinaendelea katika upatikanaji wa ripoti husika.

iv) Kuandaa program za kuhamasisha jamii kwa kuandaa Jarida la SHAHIDI.

v) Kuandaa mikutano sita ya Wadau na Waendesha Mashtaka.

vi) Kukaa Kikosi kazi kwa ajili ya Mahkama ya Rufaa. Aidha, Vikosi kazi kwa ajili ya Programu ya Maendeleo Rasilimali Watu pamoja na uanzishwaji kitengo cha kuwalinda waathirika vinafanyiwa kazi.

vii) Kuwapatia mafunzo Wafanyakazi wake watano na wengine 18 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu.

2. Kuimarisha miundombinu ya Afisi kwa kukamilisha makaazi ya Wanasheria huko Chake Chake pamoja na Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria.

3. Kuanza kazi kwa Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria kwa;

i) Kutangaza zabuni ya ununuzi wa vifaa.

ii) Kuwapatia mafunzo Wakufunzi na Watendaji.

iii) Kuandaa na kusambaza Kanuni na Miongozo ya Kituo.

iv) Kukamilisha Mpango Mkakati wa Kituo na kusubiri mapitio ya Wadau.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 774,000,000/- kati ya fedha hizo Tsh. 339,000,000/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 435,000,000/- kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Disemba, 2011 jumla ya Tsh. 288,480,300/- sawa na asilimia 37 ziliingizwa na kutumiwa. Kati ya hizo Tsh. 184,346,319/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 104,133,981/- kwa matumizi mengineyo.

Kwa upande wa Pemba - **Afisi ya Mkurugenzi Mashtaka** katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 imemudu kutekeleza malengo yake iliyojipangia kama ifuatavyo;-

a) Iliendelea na shughuli ya usimamizi na uendendeshaji wa mashtaka katika ngazi zote za Mahkama ya Mkoa na Mahkama Kuu, ambapo kesi 78 zilifunguliwa katika Mahkama ya Mkoa wa Kusini na Kaskazini – Pemba. Kati ya hizo kesi 44 zilifunguliwa Mkoa wa Kusini na kesi 34 zilifunguliwa Mkoa wa Kaskazini. Aidha, Ofisi imekuwa ikisimamia na kufuatilia kwa karibu uendeshaji wa mashtaka katika Mahkama za Wilaya zote za Pemba ambazo kwa hivi sasa mashtaka yake bado yanaendeshwa na Polisi, lengo ni kuimarisha uendeshaji wa mashtaka.

b) Imeweza kukutana na Maafisa Upelelezi na Waendesha Mashtaka wa ngazi ya Mkoa, kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kupeana maelekezo ya utendaji kazi.

c) Imeendelea kufanya kazi kwa karibu na taasisi mbali mbali zilizo na mahusiano ya kikazi na Afisi hii.

d) Imeendelea na kazi ya ujenzi wa nyumba ya Afisi iliyopo Madungu, ujenzi ambao upo katika hatua ya umaliziaji (Finishing). Mjenzi wa nyumba hiyo ni Kampuni ya ZECON na gharama halisi ya ujenzi huo ni jumla ya Tsh. 142,442,520/-. Kutokana na uhaba wa maingizo ya fedha, ujenzi wa awamu ya mwanzo ambao ulijumuisha uinuaji wa matofali hadi kuezeka tu umegharimu jumla ya Tsh. 74,820,260/-. Hivyo, jumla ya Tsh. 67,622,260/- zinahitajika kukamilisha ujenzi uliobakia.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 kiasi cha fedha kilichoingizwa na kutumika ni Tsh.78,870,399/-. Kati ya hizo Tsh. 25,290,399/- zilitumika kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 53,580,000/- zilitumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (Other Charges).

**CHANGAMOTO**

Pamoja na mafanikio makubwa yanayopatikana Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka bado inakabiliwa na changamoto kadhaa. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

1. Ucheleweshwaji wa kupatiwa fedha za matumizi ya Ofisi kwa wakati kwa upande wa Pemba ni kikwazo kikubwa kinachopelekea malengo ya Ofisi yasitekelezwe kwa wakati na pale fedha zinapoingizwa pungufu hupelekea baadhi ya malengo ya Ofisi yasitishwe.

2. Uelewa mdogo kwa baadhi ya wadau (jamii) juu ya usimamizi wa haki katika mashauri ya jinai, hususan katika suala la dhamana, kwamba dhamana ni haki ya mshtakiwa na hivyo basi pale washtakiwa wanapopewa dhamana huzuka malalamiko miongoni mwa jamii wakihoji uhalali wa watuhumiwa hao kuwepo mitaani.
3. Kutokupatikana kwa suluhisho muafaka kwa kesi za udhalilishaji wa wanawake, hasa zile kesi zinazohitaji uchunguzi wa vinasaba kwa kutumia kipimo cha DNA.
4. Ukosefu wa wataalamu katika taasisi nyengine tunazoshirikiana nazo katika utendaji wetu wa kazi wa kila siku. Mfano mzuri ni ukosefu wa Daktari maalum wa uchunguzi wa maiti (Pathologist) ikitiliwa maanani kwamba matakwa ya kisheria ni kwamba miili ya marehemu inatakiwa kufanyiwa uchunguzi na Mtaalamu wa uchunguzi wa Miili ya marehemu (Pathologist).

5. Ofisi bado inakabiliwa na tatizo la ufinyu wa nafasi kwa upande wa Pemba. Aidha, uchakavu wa jengo umekuwa ukiendelea kuwa mbaya siku hadi siku. Kwa hivi sasa hali ya jengo hairidhishi hata kidogo, hii ni kutokana na kuwa jengo limeanza kufanya nyufa ndogo ndogo katika sehemu mbali mbali za kuta zake. Hata hivyo, Afisi imeshindwa kuanza ujenzi wa Jengo la Afisi yake mpya hapo Tibirinzi kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi huo. Kwa hivi sasa Afisi ina malengo ya kupangisha eneo ambalo litakuwa na nafasi ya kutosha na jengo liliopo hivi sasa litatumika kama Kituo cha Kutolea Mafunzo (Resources Centre).

6. Kwa upande wa Pemba Ofisi hii ina jumla ya wafanyakazi 15, kati ya hao Wanasheria ni watano tu. Kwa hivi sasa Wanasheria waliopo Afisini ni wanne na mmoja yupo masomoni. Idadi hii ndogo na inakwaza ufanisi wa shughuli za uendeshaji mashtaka. Tayari Ofisi Kuu imeshaomba kuajiri Wanasheria lakini hadi sasa hawajaruhusiwa kuajiri.

7. Ingawa Serikali imeboresha maslahi ya wafanyakazi, bado mshahara wa Mwendesha Mashtaka wa Serikali haujaridhisha hata kidogo kulinganisha na majukumu mazito aliobeba.

**AFISI YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI**

Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia mwezi wa Disemba, 2012 imeweza kutekeleza malengo yafuatayo;-

1. Kuendelea Kuifanyia Marekebisho mifumo na sheria zinazoongoza usajili kwa;-
    i) Kuwasilishwa Wizarani rasimu za Sheria za Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali, Sheria ya Usajili wa Biashara na Sheria ya Kampuni kwa hatua muafaka.

    ii) Mtaalamu anayeratibu mageuzi ya mfumo wa utoaji wa leseni za biashara kukabidhi ripoti ya mwisho pamoja na marekebisho ya rasimu ya sheria hiyo.

    iii) Kuendelea na kazi ya kuupitia na kuurekebisha mfumo wa usajili wa vizazi na vifo , ndoa na talaka na uasili.

2. Kuimarisha Usimamizi na Usajili wa Tasnia ya Mali za Ubunifu kwa kuandaa vipindi vya TV na redio vitakavyoshajihisha umuhimu wa usajili wa tasnia ya mali za ubunifu. Hatahivyo, vipindi hivi vitarushwa hewani zitakapopatikana fedha.

3. Kurekebisha kasoro za utendaji zinazochelewesha upatikanaji wa vyeti na huduma nyenginezo kwa;-

    i) Kutoa ada ya kuchapishwa madaftari ya usajili wa vizazi na vifo 3,000 na madaftari ya ndoa na talaka 2,000.

    ii) Kununua Samani, Kompyuta, Typewriter, vifaa vya kuandikia na vya kompyuta pamoja na mihuri.

    iii) Kulipia huduma ya internet, safari za kikazi na huduma nyengine za kiuendeshaji.

    iv) Kuhudhuria Mfanyakazi mmoja kozi ya miezi mitatu ya "database" huko Dar es Salaam. Aidha, Afisi imelipia gharama za mafunzo kwa wafanyakazi wake watatu wanaosoma katika fani tofauti.

4. Kuimarisha mashirikiano na taasisi zote zinazohusiana na masuala ya usajili na utunzaji kumbukumbu kwa kuendelea kuzipitia kumbukumbu zilizozidi miaka 65 kwa ajili ya kuzitayarisha na kuzipeleka Idara ya Nyaraka Zanzibar.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**
Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Afisi hii iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 336,281,000/- kati ya fedha hizo Tsh. 149,344,000/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 186,937,000/- kwa matumizi mengineyo.

Hadi kufikia Disemba, 2011 jumla ya Tsh. 140,651,206/- sawa na asilimia 42 ziliingizwa na kutumiwa. Kati ya hizo Tsh. 94,534,140/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 46,117,066/- kwa matumizi mengineyo.

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011, Ofisi hii kwa upande wa Pemba imeweza kutekeleza malengo yafuatayo;-

a) Ilisambaza jumla ya vyeti 5893 vya kuzaliwa katika Wilaya zake nne za Pemba, ambavyo viligawiwa kiwilaya kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| i) | Wilaya ya Wete | 1010 |
| ii) | Wilaya ya Mkoani | 1500 |
| iii) | Wilaya ya Chake | 1587 |
| iv) | Wilaya ya Micheweni | 1796 |
| **JUMLA** | | **5893** |

b) Ilifanikiwa kununua vespa moja ili kupunguza tatizo la usafiri, jokofu moja na kiyoyozi kwa ajili ya matumizi ya Ofisi. Sambamba na hayo Ofisi hii imefanikiwa kununua samani ‘furnicher’ ili kuboresha mazingira ya ofisi kiutendaji.

c) Ili kuboresha ufanisi na uwajibikaji Ofisi inaendelea kuwasomesha wafanyakazi wake wawili (2) katika ngazi ya Diploma.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**
Katika Kipindi hiki Ofisi hii imeingiziwa na kutumia jumla ya Tsh. 33,410,824/-, ambapo Tsh. 16,810,824/- zilitumika kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 16,600,000/- zilitumika kwa ajili ya shughuli za uendeshaji (O/C).

Aidha, kwa upande wa vizazi na vifo, nyaraka, ndoa na talaka Ofisi imefanikiwa kukusaya jumla ya Tsh..10,974,000/.

**Changamoto**
Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

a) Kushindwa kuwalipia baadhi ya Wafanyakazi wake waliopo masomoni kutokana na uhaba wa fedha zilizopatikana kwa upande wa Unguja.

b) Jamii kushindwa kuelewa umuhimu wa usajili wa vifo.

c) Jumuiya Zisizo za Kiserikali kushindwa kuwasilisha taarifa zake za mahesabu kama Sheria inavyoelekeza.

d) Upungufu wa magamba ya vyeti vya kuzaliwa kitu ambacho ndio kilio kikubwa kwa wananchi pamoja na fomu za B1 ambazo hutumika kwa Masheha na Hospitali kwa upande wa Pemba.

e) Tatizo la usafiri, hadi sasa ofisi haina gari hata moja la kufuatilia shughuli za kiutendaji kwa upande wa Pemba.

**KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA**

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2012 Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imemudu kutekeleza mambo yafuatayo;-

1. Kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa mali za Wakfu na Amana kwa;-
   - i) Kufanya utafiti wa kuzitambua mali za Wakfu na Amana kwa kutumia wataalamu wa ndani na kuweka kumbukumbu sahihi. Katika kutekeleza hili jumla ya Majalada 86 yamekaguliwa na nyaraka 32 za nyumba za wakfu zimepatikana.
   - ii) Kukagua Nyumba 86 za wakfu na 2 za Amana, mashamba 6 ya wakfu na 1 la Amana.
   - iii) Kuandaa michoro ya nyumba ya ghorofa 5 ya kiwanja Namba 203. Hatahivyo, malipo hayajafanyika ingawa kazi imeanza.
   - iv) Wataalamu kuyakaguwa mashamba ya Cheju na Dunga na kushauri kwamba mashamba hayo yaendelezwe ambapo katika kipindi cha kiangazi yameendelezwa.
   - v) Kuwaelimisha wadau mbalimbali wa Kamisheni, ambapo vikao vya Wanufaika na Wapangaji viliandaliwa, vipindi kumi vya redio na viwili vya televisheni vimefanyika.
2. Kuweka mfumo bora wa shughuli za Zakka. Katika kufanikisha hili Mshauri Mwelekezi aliajiriwa kwa ajili ya kuandaa kanuni, muundo, mkakati na miongozo ya utekelezaji wa Diwani ya Zakka.
3. Kuendeleza Watendaji na Kuimarisha Mazingira ya Kazi kwa;-
   - i) Kununuliwa nakala 50 za Sheria ya Kamisheni ambapo 30 zimegawiwa kwa wadau mbalimbali.
   - ii) Kuendelea na kazi ya kutayarisha Kanuni za Hiba na Wakfu, Wasia na Mirathi , Huduma, Ada na Malipo.
   - iii) Kuandaa Mpango Mkakati wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana
4. Kuendeleza shughuli za uratibu kwa;-
   - i) Kuandaa kikao kimoja cha Bodi na vikao vitatu vya utendaji.
   - ii) Kuratibu Safari za Hijja.
   - iii) Kusimamia Sala na Mabaraza ya Iddi Kitaifa.
   - iv) Kuendelea kusimamia huduma za Msikiti wa Mwembeshauri.
   - v) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano, maji, umeme na usafiri zinaendelea kupatikana.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Kamisheni hii iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 300,000,000/- kati ya fedha hizo Tsh. 217,544,000/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 82,456,000/- kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Disemba, 2011 jumla ya Tsh. 225,834,485/- sawa na asilimia 75 ziliingizwa na kutumiwa. Kati ya hizo Tsh. 149,806,660/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 76,027,825/- kwa matumizi mengineyo.

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 **Kamisheni** hii kwa upande wa Pemba ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

a) Iliweza kusimamia mirathi ya Waislamu kwa mujibu wa Sheria. Jumla ya tirka 50 zimefunguliwa na tirka 64 zenye thamani ya Tsh. 331,940,742.40 zimefungwa na tirka 7 zinangojea uamuzi wa Mahkamani, moja iko Mahkama Kuu na sita ziko katika Mahkama ya Ardhi.

b) Iliweze kusimamia Sala na Baraza la Iddi Kitaifa.

c) Iliimarisha mfumo wa Usimamizi wa Mali za Wakf na Mali za Amana ili kuongeza ufanisi, uhifadhi na mapato yake. Katika kufanikisha hili Kamisheni imeweza kuunda timu ya Wafanyakazi kwa ajili ya utafiti wa Mali za Wakf ambazo Kihistoria zilikuwa katika dhamana ya Kamisheni ya Wakf. Lakini kutokana na sababu mbali mbali hivi sasa baadhi ya wakfu hizo zimo mikononi mwa watu kinyume na Sheria. Hivyo kwa kipindi hichi cha miezi 6 Kamisheni imeweza kugundua vipande 4 vya shamba za Wakf vya Mikarafuu na Minazi na Shamba moja la Wakf liliopo Michakaini - Chake-Chake.

d) Kitengo cha Wakf chini ya Kamisheni kimefanya ukaguzi wa nyumba za Wakf na kuangalia upya kodi za Nyumba zinazolipwa sasa na kupendekeza kodi mpya.

e) Iliwalipa fidia wanufaika watatu waliokatiwa eka shamba zao zenye thamani ya Tsh. 2,509,788.30.

f) Katika kuliendeleza shamba la Wakf la Bwagamoyo, Kamisheni iliweza kufyeka sehemu zote zenye mikarafuu tu na kupanda mikarafuu mipya 100 na minazi 220.

g) Iliendelea kuwaendeleza Watendaji wake na Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi. Katika kufanikisha hili Kamisheni – Pemba waliwapatia fursa ya kuhudhuria katika Semina elekezi wafanyakazi wake iliyoandaliwa na Kamisheni ya Wakf Zanzibar chini ya Katibu Mtendaji. Semina hiyo ilizungumzia wajibu wa Wafanyakazi, haki za Mfanyakazi na Muelekeo wa kubadilika katika utendaji wetu wa kazi.

h) Iliendelea kuwalipia Wafanyakazi wake watatu wanaoendelea na mafunzo mbali mbali katika ngazi za Advance Diploma, Degree, Diploma na Cheti.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Kamisheni ya Wakf - Pemba imeidhinishiwa kutumia Ruzuku ya Tsh. 70,050,000/- ambapo hadi kufikia Disemba 2011 jumla ya Tsh. 32,624,130/- ziliingizwa na kutumika kwa ajili ya mshahara na maposho.

**CHANGAMOTO**

Pamoja na jitihada kubwa ya utendaji inayochukuliwa, bado Kamisheni inakabiliwa na baadhi ya changamoto kama zifuatazo:-

1. Ufinyu wa Bajeti
2. Usafiri
3. Ugumu wa utekelezaji wa Sheria No. 2/2007 pamoja na migongano ya Sheria hii na Sheria nyengine mbali mbali.

**Maoni ya Kamati**

1. Kamati inaishauri Kamisheni kuzidi kufuatilia mali za Wakfu ili kuepusha dhima mbele ya Mwenyezi Mungu.

2. Tunashauri Mashamba yote ya Wakfu ijulikane mipaka yake kwa lengo la kuepusha kuvamiwa mashamba hayo.

3. Kwa kuwa mali za Wakfu zinahusiana na masuala ya dini ya Kiislamu ni vyema utekelezwaji wake ukafanywa kwa misingi ya dini hiyo. Kwa mnasaba huo tunashauri zifanyiwe marekebisho Sheria zote zinazopingana na Sheria ya Wakfu kwani imebainika kuwa mafanikio ni madogo tangu ilivyoanzishwa Sheria hii.

**AFISI YA MUFTI**

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2012 Afisi ya Mufti imeweza kutekeleza malengo yafuatayo;-

1. Kuimarisha Uratibu wa taasisi za kidini kwa;-
   i) Mufti kutembelea baadhi ya Misikiti na Madrasa Unguja na Pemba.
   ii) Kuimarisha uendeshaji bora wa Madrasa Unguja na Pemba ambapo takriban 2000 Madrasa zimetambuliwa Unguja na Pemba.
2. Kuimarisha uwezo wa Afisi kiutendaji kwa;-
   i) Kuwapatia nafasi ya mafunzo Wafanyakazi wawili.
   ii) Kuendelea kupata huduma za uendeshaji wa Ofisi, ikiwa ni pamoja na kununua vifaa vya kuandikia vya ofisi na kutengeneza gari za Ofisi.

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Afisi ya Mufti iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 140,435,000/- kati ya fedha hizo Tsh. 70,208,000/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 70,227,000/- kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Disemba, 2011 jumla ya Tsh. 76,128,503/- sawa na asilimia 54 ziliingizwa na kutumiwa. Kati ya hizo Tsh. 57,018,508/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 19,109,995/- kwa matumizi mengineyo.

Kwa upande wa Pemba Afisi ya Mufti katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2011, imeweza kutekeleza malengo yafuatayo;-

a) Ilipokea na kuyapatia ufumbuzi kwa mujibu wa sheria za kiislam jumla ya mas-ala 19 ya fatwa yanayohusu ndoa na talaka.

b) Ilitoa vibali 11 kwa ajili ya mihadhara pamoja na vibali 13 vya kuombea misaada.

c) Katika harakati za kujenga umoja na mshikamano ofisi ilipokea migogoro 19 inayohusu mashamba na ndoa kwa kuipatia ufumbuzi unaofaa, kati ya hiyo migogoro miwili ya mashamba imepelekwa mahakamani kwa kupatiwa ufumbuzi zaidi.

d) Katika kupeleka uislimu mbele ofisi imefanikiwa kusajili jumla ya vyuo 6 vya qur-an na misikiti 8.

e) Ilikutana na viongozi wa jumuiya ya kidini (JUMAZA) kwa ajili ya kuwapa miongozo mbali mbali ya utendaji wa kazi katika harakati zao.

**AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI**

Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 hadi kufikia Disemba, 2012, Afisi hii imemudu kutekeleza majukumu yafuatayo;-

1. Kuongeza kasi ya ulipiaji kazi za Hakimiliki kwa watumiaji kibiashara kwa;-

i) Kufanya ukaguzi katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi yanayotumia kazi za Hakimiliki kibiashara ambapo Ukaguzi utaendelea katika Mikoa mingine iliyobaki.

ii) Kufanya mazungumzo na watumiaji wa kazi kibiashara hususan Wamiliki wa Mahoteli. Hata hivyo, mazungumzo yanaendela na muafaka bado haujapatikana.

iii) Kukusanywa Mirabaha kutoka vituo binafsi vya Utangazaji pamoja na wakodishaji wa vinasa sauti na picha za hakimiliki.

2. Kuimarisha uwezo wa Afisi kiutendaji kwa kuandaa mafunzo ya muda mfupi kwa watendaji wa Afisi pamoja na kununua zana za kufanyia kazi na mawasiliano (kama mafuta, umeme, mtandao, na vifaa vya kuandikia).

**Hali ya Upatikanaji wa Fedha**
Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Afisi hii iliidhinishiwa jumla ya Tsh. 100,000,000/- kati ya fedha hizo Tsh. 42,625,392/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 57,374,608/- kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Disemba, 2011 jumla ya Tsh. 44,061,735/- sawa na asilimia 44 ziliingizwa na kutumiwa. Kati ya hizo Tsh. 10,201,816/- kwa ajili ya mishahara na maposho na Tsh. 33,859,919/- kwa matumizi mengineyo.

**CHANGAMOTO**
Afisi ya Hakimiliki inakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

a) Kushindwa kuandaa Rasimu ya awali ya marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki Nam.14 ya 2003.
b) Uhaba wa watendaji hususan Pemba

**OFISI KUU PEMBA**
Ofisi Kuu Pemba ni kiungo muhimu katika kuunganisha Idara na Taasisi zake kwa upande wa Pemba kwa mashirikiano makubwa yanayotolewa na Ofisi Kuu Unguja.

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2011 Ofisi hii imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo;-

a) Iliandaa mkutano na wakuu wa maidara kwa lengo la kuhamasisha uwajibikaji na ufuatiliaji wa majukumu pamoja na kusisitiza utekelezaji kwa mujibu wa mpango kazi.

b) Iliandaa mkutano uliowashirikisha wafanyakazi wa kawaida pamoja na Maofisa Utumishi wa Maidara, kuhusiana na suala zima la maslahi ya wafanyakazi na marekebisho ya mishahara kwa mujibu wa toleo jipya la Serikali pamoja na kusikiliza maoni na malalamiko yao mbali mbali kuhusiana na uimarishaji na uendeshaji wa ofisi kwa lengo la kuyapatia ufumbuzi na kujenga ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

c) Ilifanikiwa kusuluhisha migogoro mbali mbali kwa baadhi ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali ‘NGO’s. Aidha, ilizisaidia Jumuiya mbali mbali kuandaa Katiba kwa lengo la kupata usajili, pamoja na kutoa miongozo juu ya usimamizi na matumizi sahihi ya fedha kutoka kwa wahisani na namna ya kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha hizo.

d) Iliendelea kuwalipia ada ya masomo wafanyakazi wake walioko masomoni katika ngazi ya Diploma.

e) Ilifanikiwa kununua vespa mbili (2) ili kuimarisha shughuli za ufatiliaji na kazi za kawaida za ofisi. Aidha, Ofisi iliifanyia matengenezo jengo la ofisi kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya kazi.

**Changamoto**
Katika kipindi husika Ofisi Kuu Pemba imeshindwa kutekeleza baadhi ya malengo ambayo imejipangia kuyatekeleza. Miongoni mwa malengo hayo ni pamoja na;-

a) Kununua baadhi ya vifaa vya Ofisi.

b) Kuandaa baadhi ya mikutano pamoja na huduma ya kuaminika ya mawasiliano.

c) Usafiri ambapo mpaka sasa ofisi ina gari moja tu ambayo inatumiwa na Afisa Mdhamini, hali ambayo inapelekea shughuli za ufuatiliaji kupungua.

**Hali ya upatikanaji wa fedha**
Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2011, Ofisi Kuu Pemba imeingiziwa jumla ya Tsh. 116,944,980/-, kati ya hizo Tsh. 71,482,980/- ni mishahara na maposho na Tsh. 45,462,000/- ni matumizi mengineyo.

## SEHEMU YA NNE
## HITIMISHO NA MAONI YA UJUMLA YA KAMATI

Kamati ilitekeleza vyema majukumu yake ya kufuatilia utendaji wa Serikali katika mwaka wa fedha 2011/2012 kwa Taasisi za Unguja na Pemba. Ingawa ufuatiliaji huo ulikuwa ni wa miezi saba yaani kuanzia Julai hadi Disemba, 2011, hii ni kutokana na ratiba za kazi za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Kamati inapenda kutoa shukurani zake za dhati kwa Watendaji wote ambao kwa namna moja au nyengine walishirikiana nayo kutoka mwanzo hadi mwisho.

Kimsingi, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaiomba Serikali kuzidisha juhudi katika kutekeleza majukumu yake. Tunashauri hili baada ya kubaini kuwa bado kuna mapungufu ya kiutendaji kwenye baadhi ya Taasisi zake hali ambayo huviza utendaji. Maoni ya ujumla ya Kamati ni kama yafuatayo;-

- Ufinyu wa bajeti; Kamati imebaini kuwa kilio kikubwa cha Wizara zilizochini yake ni ufinyu wa bajeti, jambo ambalo huviza utendaji. Hivyo, tunaiomba Serikali kuzipatia fedha tena kwa wakati na kulingana na mahitaji yao Taasisi hizi ili ziweze kutekeleza vyema majukumu yao.

- Uhaba wa Watendaji kwa baadhi ya Taasisi; Kamati hii inaiomba Serikali kutoa nafasi za ajira kwa kuwa baadhi ya Watendaji hutoa huduma kwa zaidi ya Kituo kimoja jambo ambalo huzorotesha utendaji.

- Kutokana na uhaba wa fedha zinazopatiwa Taasisi za Serikali na kwa kuwa Watumishi wengi wa Umma wanamwamko wa kusoma, Kamati ya Katiba Sheria na Utawala inaishauri Serikali kuanzisha mfumo wa ‘cost sharing’ ili Watumishi wenye hamu ya kusoma kupata nafasi hiyo.

- Ukosefu wa usafiri; Kamati inaishauri Serikali kuzipatia Taasisi zake vyombo vya usafiri ili Taasisi hizi ziweze kutekeleza majukumu yao bila ya usumbufu wowote. Hii ni kutokana na kuwa takriban Taasisi nyingi za Serikali zinakabiliwa na changamoto hii.